



Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 DISEMBA, 2023 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 01- 10 JANUARI, 2024

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 21-31 DISEMBA, 2023

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika. Hali hii iliendelea kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kusogea kuelekea kusini na kuwepo katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani liliendelea kuwepo katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi wakati joto la bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani liliendelea kuwepo katika eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi. Hali hii iliendelea kusababisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 DISEMBA, 2023

Viashiria vya hali ya hewa tajwa hapo juu vilipelekea maeneo machache ya nchi yetu kupata vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi hasa katika maeneo ya pwani ya kaskazini, nyanda za juu kusini magharibi, ukanda wa Ziwa Viktoria na magharibi mwa nchi. Hata hivyo, vipindi vya mvua nyepesi hadi za wastani viliripotiwa katika maeneo ya kati mwa nchi, nyanda za juu kaskazini mashariki, kusini na maeneo ya pwani ya kusini.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 01-10 JANUARI, 2024

2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 JANUARI, 2024

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuimarika. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kuwepo katika baadhi ya maeneo ya kusini mwa nchi yetu. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi wakati joto

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

la bahari la wastani linatarajiwa kuwepo katika eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu. Kwa upande mwingine, katika eneo la magharibi la nchi, upepo unatarajiwa kuvuma kutokea Magharibi, hali ambayo inatarajiwa kusababisha kuletwa kwa unyevunyevu kutoka misitu ya Kongo na hivyo kuchangia kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo yaliyopo magharibi ya nchi yetu hususani katika nusu ya kwanza ya dekad.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 JANUARI, 2024

Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara): Mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro): Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Imetolewa na;

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz